336/2
KISWAHILI
Karatasi ya pili
Saa mbili

*Uganda Certificate Of Lower Secondary Education*

S.4 PRE-UNEB ASSESSMENT SET ONE

KISWAHILI

Karatasi ya pili

Ufahamu na Uchambuzi wa Fasihi

Saa mbili

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA:**

- ✓ *Karatasi hii ina sehemu mbili: A na B*
- ✓ *Maswali yote ni ya lazima.*
- ✓ *Majibu yote yaandikwe kwenye karatasi uliyopewa.*

©WESLAB 2025
Download research notes & assessments from our website
wunnaeducationservices.com

Pindua

## SEHEMU YA A: UFAHAMU

Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata:

### FAIDA ZA MICHEZO

Michezo ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Michezo inawasaidia watu kuishi bila magonjwa hususani yale yasiyoambukizwa. Unapotembelea sehemu mbalimbali ulimwenguni utaiona michezo tofautitofauti. Lakini, michezo mikubwa inayojulikana ni mpira wa miguu, mpira wa kikapu, mpira wa wavu,kuogelea na michezo ya riadha. Michezo hii ina washiriki wengi kuliko michezo mengine.

Michezo ina faida nyingi kwa binadamu yeyote awe mdogo, mtu mzima au mzee. Michezo hujenga mwili wa binadamu na kuufanya uwe mkakamavu. Mwili unaweza kuimarishwa na chakula unachokula lakini pia michezo huimarisha mwili zaidi. Unapochunguza vizuri utawaona watu ambao hawafanyi mazoezi ya michezo wakiwa na miili isiyo na nguvu ya kutosha. Kama mtu hana nguvu kwa kiwango hiki mwili wake huweza kupatwa na magonjwa mbalimbali kwa urahisi. Michezi ni njia moja ya kujilinda na magonjwa kama vili kisukari, shinikizo la damu, mfadhaiko, unene wa kupindukia, na kadhalika.

Michezo hufurahisha wachezaji wenyewe na hata watazamaji. Mtu anapocheza hufurahisha nafsi yake na kustarehesha roho yake mwenyewena kuburudisha mwili wake. Hali kadhalika, michezo huwachangamsha watazamaji na kuwafurahisha kila wanapoitazama. Mashabiki wengi hupenda kuitazama michezo mbalimbali kwa kujifurahisha na kujistarehesha. Kwa hiyo, wao huweza kunufaika pia kwani kupumzika ni jambo muhimu sana katika maisha ya binadamu. Unapopata muda wa kupumzika na kijistaresha unaweza kuongeza kiwango chako cha kufikiri na uwezo wako wa kutenda kazi kwa ufanisi. Aidha. Unaweza hata kusuluhisha matatizo muhimu yanayojitokeza katika maisha ya kila siku.

Michezo pia hujenga uhusiano mwema kati ya mtu na mtu, wilaya na wilaya, na hata taifa na taifa. Kunapokuwa na mchezo wa kimataifa, wachezaji wa timu ya taifa moja hukutana na wachezaji wa timu nyingine na kujenga uhusiano wa karibu. Urafiki baina ya watu wengi huweza kuanzia michezoni. Ili kuielewa vizuri suala hili, chunguza vizuri idadi ya watu wanaokuja kuitazama michezo katika eneo unapoishi. Mtazamaji mmoja akaapo na mtazamaji mwingine

©WESLAB 2025
Download research notes & assessments from our website
wunnaeducationservices.com

hawawezi kumaliza vipindi vyote vya mchezo bila kuambiana mambo kadhaa kuhusu mchezo huo. Watu wawili wasiofahamiana huweza kukutanishwa na mchezo wa timu yao na kuanzisha urafiki unaoweza kuwachochea kuanzisha pia miradi mingine ya kudumisha ushirikiano na mshikamano baina yao. Mathalani, mtu huweza kusifika katika nchi yake au kiwango cha kimataifa kwa kuwa mchezaji hodari katika mchezo wa kukimbia,kucheza mpira, kuendesha baiskeli, kuogelea, ndondi, mieleka na michezo mingine. Mtu akipata sifa kama hizo, hufurahia na kuridhika moyoni mwake. Aidha sifa hizi huweza kumnufaisha anyecheza michezo hiyo kwa kumletea pato kubwa kiasi cha kuwa tajiri. Taifa nalo hujulikana na kupata sifa kutokana na uhodari wa raia wake ambaye ni mwana michezo.

Kutokana na faida hizo zilizotajwa, tunapaswa kulitilia maanani suala la michezo duniani ili tuwe na maisha mema. Tujenge miili yetu kwa kucheza michezo ya aina mbalimbali hata kama hatuna uhodari wa kutosha kutokana na michezo Fulani.

Tujistareheshe na kupumzisha akili zetu kwa kucheza michezo hata kama hatuna uwezo mkubwa katika michezo hiyo. Tujenge uhusiano mwema kati yetu kwa kushiriki katika michezo mbalimbali.

**Maswali:**

Michezo ina faida gani kwa binadamu? Taja faida tatu.

Ni madhara gani yanyoweza kupata mtu asiyecheza?

Ni namna gani urafiki kati ya mtu na mtu unavyoweza kuanza michezoni?

Fafanua aina nne za michezo zilizozungumziwa katika kifungu cha habari hiki.

Ni vipi taifa huweza kunufaika kutokana na michezo?

Mtu anafaidika vipi kwa kujistarehesha na kupumzika?

©WESLAB 2025

**Download research notes & assessments from our website**

wunnaeducationservices.com

## SEHEMU B

## UCHAMBUZI WA FASIHI

**DIAMOND**: Tafadhali Zari. Huyu ndiye yule msichana nilikuambia nataka kumuoa.

**ZARI**: (Akitaka *kumpiga kofi, lakini Diamond anamshika*) Niache!! Niache! Nimwonyeshe huyo msichana wako. Hebu mwangalie ni mweusi kama makaa na makalio yake kama "flat screen"

**DIAMOND**: (Anajaribu *kuleta amani kati yao*) Unajua Zari, nilifikiri itakuwa vizuri sisi sote watatu tukutane ili tuelewane vizuri. Tafadhali wacha matusi.

**ZARI:** *(Akivuta pumzi na kuhema*). Hakuna haja ya kuelewana. Ninawaomba nyote mtoke hapa haraka. Litoe hili Malaya lako humu ndani, tena upesi.

**PINDUA**

**ZUCHU**: (*Kwa hasira*) Malaya? Mimi Malaya? Chunga ulimi wako mwamamke wewe. Una nini kunizidi mimi hapo ulipo, hata nishindwe kuwa mke wa Diamond. Kama ni elimu nimesoma hadi chuo kikuu. Kama ni kazi, mimi ni mwimbaji tena nina pesa nyingi. Wewe kazi yako ni kukaa nyumbani kumngojea Diamond akuletee pesa. Mtaka cha mvunguni ni sharti ainame.

Usiniite kahaba tena. (Zari *anamrukia. Wanashikana kupigana, bali Diamond anaingilia kati upesi kuwatenganisha)*

**DIAMOND**: Ngoja, ngoja,ngoja. Wacheni! Hasira huleta hasara. Nyote wawili ni bibi zangu. Wewe Zari ni mke wangu wa kwanza. Lakini sikusema utakuwa mke wangu wa pekee.

**ZARI**: Ee! Mungu wangu nisaidie. Shetani gani ameingia katika familia yangu. Mume wangu ambaye nimempenda sana maisha yangu yote. Nimezaa naye watoto wannne wasichana. Haya tokeni nje. Haya yamenitosha.

**DIAMOND**: (*Anamshika Zuchu pole pole na kumsaidia kuketi kwenye kiti*) Nataka muelewane wewe na Zuchu huyu, ambaye atakuwa mke

©WESLAB 2025
Download research notes & assessments from our website
wunnaeducationservices.com

mwenzako. (Anajipiga *kifua na kujigamba*). Kwa mtu mwenye mali kama mimi: mtu anayetaka kuwa mbunge wa eneo la Mityana, hakuna shida kuoa mke wa pili au wa tatu ama zaidi.

**ZARI**: *(Anasimama, anashika kiuno na kuelekeza kidole chake kwa Zuchu*) Wewe! Wewe ni mwanamke uliye na bahati sana. Umempata mwanamke mpenda amani, mnyenyekevu na mwenye subira. Waswahili wana methali isemayo: "ukiona vyaelea vyaundwa". Vitu vyote unavyoona hapa,runinga, friji, zulia, makochi na mali yote uavyoona na usivyooona , tilivitengeneza. Tulivitengeneza, mimi na huyu bwana, mume wangu, ambaye waelekea kuwa umemwangukia kufa. (*kwa mkazo*) siwezi kukuruhusu kuingia kati yetu, kuvunja nyumba yetu na kutuharibia maisha yetu kabisa. Mtoto wa juzi kama wewe, enda ukatafute tineja mwenzio mkajenge maisha yenu. Na kwa mara ya mwisho kabla sijawaonyesha kilichomkataza kuku kukojoa, naomba wewe na jibaba lako mtoke. Sitaki kuwaona humu nyumbani mwangu……. (Diamond na Zuchu wanatoka nje. Zari anabaki peke yake sebuleni na kuanza kuimba)

**Akili itazunguka, zunguka, zunguka**
**Itazunguka ukiniacha mwenzako,**
**Maana nitaumbuka,umbuka ,umbuka,umbuka**

**Nitaumbuka, yote kwa ajili yako hee!**

**Kwikwi kwikwi, nitalia!**
**Kwikwi kwikwi, ukiniachilia**
**Kwikwi kwikwi, nitaliaaa!**
**Kwikwi kwikwi, sio kwa unavyonipatia.**

**Maswali:**

Eleza sifa tatu za wahusika wowote katika dondoo hili.

Chambua mbinu za uandishi zilizotumiwa katika dondoo hili.

Kwa maoni yako, kwanini Diamond alitaka kuoa mke wa pili.

Eleza shida zozote tano ambazo wanawake wanapata katika ndoa.

Unajifunza nini kutokana na dondoo hili?

***MWISHO***

**©WESLAB 2025**
**Download research notes & assessments from our website**
wunnaeducationservices.com